Haki za Binadamu British Columbia:
Ubaguzi wa Umri

Karatsi hii ya ukweli imetengenezwa ili kukusaidia kuelewa maana ya ubaguzi wa umri hapa BC. Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na **BC Human Right Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu)**. Maelezo zaidi kuhusu mawasiliano yanapatikana mwishoni mwa karatasi hii ya ukweli.

British Columbia ina sheria ya kulinda na kukuza haki za binadamu. Hii inaitwa *BC Human Rights Code* au *Code (kanuni)*. *Code (kanuni)* inakulinda dhidi ya kutendewa mabaya au kunyimwa mafao kwa sababu ya umri wako. Inakuruhusu kuripoti lalamiko kwenye **BC Human Rights Tribunal (mahakama ya BC Human Rights)** ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa.

Code (kanuni) hii pia inakulinda dhidi ya kulipizwa kisasi ikiwa umeripoti, au unafikiria kuripoti, lalamiko au umehusika kwa njia yoyote ile. Kulipiza kisasi ni kama kuna mtu anajaribu kukudhuru au kujaribu kukufuatilia kwa nia ya kukudhuru au kukulipiza.

Je, ubaguzi wa umri ni nini?

Ubaguzi wa umri ina maana kumtendea mtu mabaya au kumnyima mafao kwa sababu ya umri wake. Ni muhimu kutambua kwamba *Code (Kanuni)* inalinda dhidi ya ubaguzi wa umri kwa watu walio kuwa na umri wa miaka 19 na zaidi pekee.

Ubaguzi wa umri unaweza kujumuisha kumnyima mfanyakazi mzee fursa ya mafunzo au kumnyima mfanyakazi kijana cheo kwa sababu anaonekana mdogo sana.

Ubaguzi kazini

Muajiri hawezi kukataa kumhoji, kumwajiri, kumuendeleza au kumfukuza mfanyakazi yoyote ikiwa sababu ni umri (miaka 19 na kuendelea).

Muajiri hawezi kufanya swala la umri liwe jambo kubwa au kutoa tangazo ya umri fulani wakati wa kuajiri. Kwa mfano, tangazo halitakiwi kusema " vijana wanatakiwa"

Wakati wa kuajiri, muajiri anaweza kuuliza ikiwa una umri wa kuruhusiwa kisheria kufanya kazi. Lakini muajiri hawezi kuuliza chochote cha kugundua umri wako kama vile " mwaka gani umemaliza shule ya sekondari"?

Baada ya kuajiriwa, muajiri anaweza kuwa na mahitaji ya kihalali ya kujua umri wa mfanyakazi kwa madhumuni ya kuandikisha katika pensheni au mpango wa mafao.

Ubaguzi katika makazi ya kukodisha

Kwa ujumla, mwenyenyumba hawezi kukataa kukukodishia nyumba kwa sababu ya umri wako. Na pia hawezi kukufukuza kwa sababu ya umri wako. Kwa mfano, mwenyenyumba hawezi kukataa kukodisha makazi ya kuishi kwa mtu mwenye miaka kati ya ishirini na thalathini ikiwa sababu kwamba mwenyenyumba anadhani vijana wanamakelele.

Kuna wakati mwingine kutambua umri inaruhusiwa kama vile:

- Mwenyenyumba anaweza kuzuia upangaji wowote isipokuwa kwa watu wenye miaka 55 na zaidi katika nyumba za wazee.
- Mwenyenyumba ana haki ya kukataa kukodisha kwa sababu yoyote ikiwa mpangaji atagawana matumizi ya jiko au choo pamoja na mwenyenyumba.

Malazi, Huduma na Vituo vya Manufaa

Mtu au biashara ambayo inatoa huduma kwa wananchi haiwezi kubagua mtu kwa sababu ya umri, miaka (19 au zaidi). pamoja na:

- malazi ya muda mfupi, kama vile chumba hotelini
- migahawa au maduka
- huduma za serikali na usafiri
- vituo vya burudani au vituo vingine vya mafao ya wananchi

Mifano ya ubaguzi kulingana na umri:

- sehemu ya kambi haiwezi kutoza kikundi cha wenye miaka 20 dola 100 amana ya uharibifu bila ya kutoza kiasi hicho hicho kwa watu wazima.
- ofisi ya daktari haiwezi kukataa kuchukua mgonjwa mzee kwa sababu " watu wazee wana matatizo mengi ya kiafya na huwa wanachukua muda mrefu sana"

Wajibu wa kujumuisha

Wajibu wa kujumuisha ina maana ya kuwa kuna wajibu wa kisheria wa kurekebisha sera, utendaji au huduma ili kukidhi mahitaji ya mtu kwa sababu ya umri wake. Kwa mfano, mahitaji ya mtu mzee yanayotakiwa ni kufanya mabadiliko na kurekebisha njia za kawaida za utendaji. Kukataa kuchukua hatua za kutosha za kukidhi mahitaji maalum ya mtu mzee inaweza kuwa ubaguzi, bila kufanya marekebisho ya mahitaji hayo itasababisha **ugumu usio kuwa na maana**.

Nitajuaje kama nina malalamiko ya Haki za Binadamu?

Kuripoti malalamiko kwenye *BC Human Rights Code (Kanuni ya haki za binadamu BC)*, **yote yafuatayo** lazima yawe ya kweli:

- umetendewa ubaya au umenyimwa mafao.
- kuna uhusiano baina ya namna ulivyotendewa (vibaya au umenyimwa mafao) na umri wako.
- Vitendo hivyo viwe vimetokea katika sehemu kama vile kazini, dukani au mgahawani, au baina ya mwenye nyumba na mpangaji.

Lazima uripoti malalamiko yako katika muda wa miezi sita ya tukio kutokea. (Kumbuka: kuna baadhi ya kesi za kipekee zisizo fuata muda huo uliyowekwa.) Kuripoti lalamiko kuanzisha mchakato wa kisheria sawa na hatua za hakama. Mtu mwenye kuripoti malalamiko anaitwa **mlalamikaji.**

Kwa maelezo ya ujumla kuhusu Human Rights katika BC (Haki za Binadamu BC), tafadhali tazama karatasi ya ukweli kuhusu ***Haki za binadamu British Columbia: Nini unahitaji kujua***.

Wapi naweza kupata usaidizi?

Walalamikaji popote katika jimbo wanaweza kupata maelezo kupitia **BC Human Rights Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu)**. Watu wa kliniki wanaweza kukusaidia kuelewa *Human Rights Code (Kanuni za Haki za Binadamu)* au kushughulikia malalamiko ya haki za binadamu ya jimbo. Unaweza pia ukafuzu kupata aina tafauti za huduma. Zungumza na mtu yoyote katika kliniki ili uone ikiwa utakubaliwa.

Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu

300-1140 West Pender Street, Vancouver, B.C. V6E 4G1
Phone: 604 622-1100 Toll Free: 1 855 685-6222
Fax: 604 685-7611
Online: www.BCHRC.net

Ikiwa kuna mtu amefanya malalamiko juu yako, basi wewe ni **mhojiwa**. **Wahojiwa** wote kwenye jimbo na eneo la Victoria wanaweza kupata maelezo zaidi kwa kuwasiliana na:

University of Victoria

Law Centre Clinical Law Program
Suite 225 – 850 Burdett Avenue, Victoria, B.C. V8W 1B4
Phone: 250 385-1221 Toll Free: 1 866 385-1221
E-mail: reception@thelawcentre.ca

Unaweza kuelekezwa kwa **BC Human Rights Tribunal (Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu)** kuwasilisha malalamiko yako.

Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu

Suite 1170 – 605 Robson Street, Vancouver, B.C. V6B 5J3
Phone: 604 775-2000 Toll Free: 1 888 440-8844
TTY (walio kuwa na matatizo ya kusikia): 604 775-2021
Online: www.bchrt.gov.bc.ca

Karatsi hii ya maelezo imekusudiwa kwa madhumuni ya kutoa maelezo kwa ujumla tu. Siyo kwa nia ya kuchukuwa nafasi ya ushauri wa kisheria.